23 tani
ka kwa

... na soko likiwepo
litawanyanyua wakulima
kiuchumi.

* HABARI LEO UK 19 *

# Wazalishaji chakula cha mifugo wasiosajili matatani

**Na Lucy Ngowi**

MSAKO dhidi ya wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo wasiofuata sheria na kanuni zinazoongoza utekelezaji wa shughuli hizo utaanza hivi karibuni.

Kauli hiyo imetolewa na Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA) iliyoko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Stella Bitanyi.

Dk Bitanyi aliwataka wazalishaji wa chakula cha mifugo kuhakikisha wanapeleka sampuli kwenye maabara kuu ya Veterinari ambao ndio wenye ithibati ya kitaifa ya kuchambua vyakula vya mifugo ili kuthibitisha na kutoa vyeti vya ubora.

Pia aliwataka wazalishaji kuhakikisha wanapima malighafi wanazotumia kutengeneza vyakula vya mifugo na kusajili taasisi na mahali wanapozalishia vyakula hivyo.

Dk Bitanyi pia aliwataka wauzaji wa vyakula kununua vyakula hivyo kwa wazalishaji waliothibitishwa kwenye viwango vya ubora kwa kila kundi la chakula wanalotaka kununua.

Naye mzalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka mkoani Pwani, Samson Maro alisema serikali imefanya jambo zuri kwa kufanya msako huo kwani unasaidia kuwaepusha na madhara ya kibiashara.

Uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini unasimamiwa na Sheria ya Nyanda za Malisho na Chakula cha Mifugo ya mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2013.